

miaka 20 ya Mpango wa dharura wa Rais wa Marekani wa kudhibiti maambukizi ya virusi vya Ukimwi (PEPFAR) mwishoni mwa wiki. (Picha na Alexander Sanga).

HABARI LEO UK 19

# \* Wafugaji wafurahishwa 'kopa ng'ombe lipa maziwa'

Na Diana Deus, Karagwe

JAMII ya wafugaji wilayani Karagwe Mkoa wa Kagera wameanza kunufaika na mradi wa 'Kopa Ng'ombe Lipa Maziwa' unaotekelezwa na Kiwanda cha kusindika maziwa cha Kahama Fresh.

Lengo la mradi ni kuisaidia jamii hiyo kufuga kwa tija, ambapo wanufaika wanakopeshwa ng'ombe wa kisasa na kuuza maziwa kwa mkopeshaji.

Wanufaika waliiambia Habari-LEO juzi kwamba kila mwanachama ambaye amepatiwa mafunzo ya ufugaji bora anakopeshwa ng'ombe mwenye mimba, anapozaa mkopaji anafanya marejesho kwa kukiuzia

kiwanda maziwa.

"Kwenye thamani ya maziwa hayo tunayopeleka, mkopeshaji anakata asilimia yake na kutuachia sisi kiasi tuendeshee maisha. Anayezingatia kanuni za ufugaji bora anaweza kumaliza marejesho ndani ya miaka miwili na ng'ombe kuwa mali yake," alisema mmoja wa wanufaika wa mradi Roberth Rwenkome.

Alitoa pongezi kwa serikali kuweka mazingira bora ya uwekezaji, kwani mbali na kiwanda kuwakopeshwa ng'ombe, kitaendelea kuwa soko la kudumu kwao.

Mradi huo unawanufaisha pia wazalishaji malisho ya mifugo, ambao wamepata soko la kudumu la malisho kwa wafugaji wanaoko-

peshwa ng'ombe.

Mzalishaji malisho, Erick Kagoro alisema pamoja na kuuza malisho, mradi unawaweka karibu na wafugaji na kufundishwa mbinu za ufugaji bora, hatua inayowashawishi na wao kufuga.

"Pia tunahakikishia malisho yapo katika kiangazi na masika. Tunaboresha malisho kwa kuongeza vitamini ili mifugo ya wateja wetu itoe mazao bora na sisi tuendeleo kuwa na soko," alisema.

Mkurugenzi wa Kahama Fresh, Jossam Ntangeki alisema jamii inapaswa kukamata fursa katika sekta ya kilimo na ufugaji, huku wahitimu wa vyuo wakitumia ujuzi wao kujiajiri kupitia 'Kopa Ng'ombe lipa Maziwa', mradi ambao ni endelevu.

\*

Kat

Ali

Wa

na m